

**TAARIFA YA ZIARA YA KUKAGUA MAENDELEO YA MRADI WA UWEKEZAJI ANAYEOMBA  
KUWA NA HADHI YA MWEKEZAJI MAHIRI TAREHE 2-08-2022**

**MRADI WA UPANUZI WA SHAMBA LA MIWA NA KIWANDA CHA KUZALISHA SUKARI CHA  
KILOMBERO SUGAR COMPANY LIMITED**

Na.	HADIDU ZA REJEA ZILIZOTOLEWA	UFAFANUZI/MAELEZO YALIYOTOLEWA	MAONI YA TIMU
1.	Kupata maelezo ya jumla ya utekelezaji wa mradi na kuangalia hatua iliyofikiwa.	Mradi wa upanuzi wa kiwanda hiki unafanyika ili kuongeza uzalishaji wa sasa kwa kiwanda mama kilichojengwa hapo awali (mnamo mwaka 1962) katika eneo la kilombero maarufu kwa jina la K1. Upanuzi wa kiwanda unafanyika eneo la kilombero 4 (K4) ambapo kazi inaendelea na imefikia hatua ya asilimia 22.	Kazi inaendela kwa kasi kwa kutengeneza miundombinu ya barabara inayojengwa kwa mawe. Utekelezaji wa mradi huu unaridhisha.
2.	Mwekezaji awasilishe mpango wa utekelezaji wa mradi wa K4	Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kwa awamu moja tu. Mwekezaji ametawanya utekelezaji wa kazi hii katika maeneo mawili ambayo ni eneo la mradi lenyewe (on show activities) na kazi nyingine (off show activities) zinazofanyika kupitia viwanda vya nje ya nchi ikiwa ni pamopja na utengenezwaji wa mashine na vifaa	Mradi huu utakapokamilika utawezesha kupunguza uhaba wa sukari kwa kuzalisha shukari kiasi cha tani 271,000 kwa mwaka.

		<p>vingine hitajika kutoka nchi za India, South Africa, Brazil na China vinavyotarajiwa kusafirishwa kuletwa hapa nchini kuanzia mwezi Septemba, 2022. Utekelezaji wa mradi huu mpaka sasa umefikia asilimia 22 na mradi huu unatarajia kukamilika mwezi Juni, 2024.</p>	
3.	<p>Upatikane ufafanuzi kuhusiana na umiliki wa ardhi kwa sasa katika eneo la upanuzi wa mradi</p>	<p>Ardhi iliyotengwa kwa ajili ya upanuzi wa mradi huu ni hekta 13 kutoka katika hekta 10,000 zinazomilikiwa na Kampuni ya Kilombero. Eneo hilo lilikuwa linalimwa miwa hivyo kuamua kuing'oa na kujenga kiwanda cha sukari.</p>	
4.	<p>Kupata ufafanuzi wa maombi ya mwekezaji ya kusamehewa ushuru wa mafuta aina ya dizeli kiasi cha lita 800,000, lita 20,000 za mafuta ya injini na lita 7,000 za vilainishi ni kwa matumizi gani? Na pia kupata ufafanuzi wa muda wa utekelezaji wa mradi huu.</p>	<p>Mafuta ya dizeli na vilainishi yanahitajika kuanzia wakati wa ufungaji na majaribio ya mitambo. Na pia wakati anapoendelea na uzalishaji wakati mitambo na mashine vikiwa bado kwenye kipindi cha majaribio na matazamio.</p> <p>Muda wa utekelezaji wa mradi ni kati ya miaka 5 - 7</p>	
5.	<p>Kupata ufafanuzi kutoka kwa mwekezaji kuhusiana na kutolewa msamaha wa zuio (withholding taxes) kwa huduma na ushauri wa kitaalam kutoka nje</p>	<p>Mitambo na mashine zilizofungwa ama zinazotarajiwa kufungwa huagizwa nje ya nchi. Hivyo</p>	

	<p>kwa muda wa miaka saba (aina ya ushauri kutoka nje anayoiomba).</p>	<p>ufungaji na matengenezo ya aina yoyote hufanywa na wataalam kutoka nje (mtengenezaji). kufuatana na mkataba. Mwekezaji anapaswa kuzuia asilimia kumi na tano (15%) kama kodi ya zuio pindi anapofanya malipo kwa ajili ya huduma ya utaaalam. Hatua hii inamwongezea gharama mwekezaji kwa kuwa wataalam hao nao huongeza asilimia 15 kwenye madai yao ili kufidia gharama za kodi ya zuio.</p>	
<p>6.</p>	<p>Kupata ufafanuzi kuhusu muda wa kupatiwa msamaha kwa kupata nyongeza ya idadi ya vibali vya kazi na ukaazi kwa wataalam wa kigeni.</p>	<p>Vibali vya nyongeza vinavyoombwa ni kwa ajili ya wataalam watakaokuja kufunga mashine na vifaa vya kisasa kutoka nchi ambazo zimetengeneza mashine na vifaa hivyo ambazo ni China, India, South Africa na Brazil kwa muda wa miaka mitano mpaka saba ambapo mitambo hiyo itakuwa imefanyakazi kisawa sawa. Mwekezaji ameeleza kwamba kwa vile teknolojia inayotegemewa kutumika ni mpya, uhitaji wa wataalam hawa hauepukiki</p>	<p>Kwa vile teknolojia itakayotumika kwa mujibu wa michoro na ramani vilivyooneshwa, ipo haja ya kuangalia namna ya kusaidia kuharakisha vibali vya kazi kwa wataalm hawa kwa mujibu wa sheria za kazi nchini.</p>

		isipokuwa watakuwa wanafanyakazi sambamba na watanzaia ili kupata uzoefu.	

Tunaomba kuwasilisha

**J.M.Baitu,**  
**L. Mapunda**  
**Steven Mkama**  
**3-8-2022**